



**Global Storybooks**


[globalstorybooks.net](http://globalstorybooks.net)

## Kuku na Tai

✎ Ann Nduku

👤 Wiehan de Jager

📄 Matteo E. Mwita



This work is licensed under a Creative Commons Attribution 3.0 International License.  
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>



## Kuku na Tai



✎ Ann Nduku

👤 Wiehan de Jager

📄 Matteo E. Mwita

|| 3

🗨️ Kiswahili! MS




Hapo zamani za kale, Kuku na Tai walikuwa marafiki. Waliishi kwa amani na ndege wengine. Hakuna kati yao aliyeweza kupaa.



Kila kivuli cha mabawa ya Tai kinapoonekana ardhini, Kuku huwatahadharisha vifaranga vyake. "Tokeni kwenye eneo la wazi." Na wanajibu: "Sisi si wajinga. Tutakimbia."

Kuna siku njaa ilitokea. Ikamlazimu Tai kutembea umbali mrefu kutafuta chakula. Alirudi akiwa amechoka sana. "Lazima kuwe na njia rahisi ya kusafiri!" Tai alisema.



Tai aliporudi siku iliyofuta, alimkuta kuku akichakura mchangani, ila hakukuwa na sindano. Kwa hiyo Tai alishuka kwa kasi na kukwapua kifaranga kimoja. Akaondoka nacho. Tangu hapo, kila Tai anapojitokeza humkuta kuku akichakura kwenye mchanga akitafuta sindano.





Baada ya usingizi mnono wa usiku,  
Kuku alijiwa na wazo zuri sana.  
Akaanza kukusanya manyoya  
yaliyodondoka kutoka kwa ndege  
wenzao. "Tuyashonee haya  
manyoya juu ya manyoya yetu,"  
Kuku alisema. "Labda itaturahisishia  
kusafiri."



"Nipatie siku moja," Kuku  
alimwomba Tai. "Halafu utaweza  
kushona bawa lako na kuruka tena  
kwenda kutafuta chakula." "Siku  
moja tu," alisema Tai. "Kama  
hutaipata sindano, itabidi unipe  
kimoja cha vifaranga vyako kama  
malipo."

Tai pekee ndiye aliyekuwa na sindano kijijini, kwa hiyo akaanza kushona wa kwanza. Akajitengeneza mabawa mawili mazuri na akapaa juu ya kuku. kuku aliazima sindano lakini akachoka kushona baada ya muda mfupi. Akaacha sindano kabatini na akaenda jikoni kuandaa chakula kwa ajili ya watoto wake.



Baadaye jioni Tai akarudi. Akaomba sindano ili aweze kushona baadhi ya manyoya yaliyokuwa yameanza kulegea alipokuwa safarini. Akaangalia kwenye kabati. Akaangalia jikoni. Akaangalia uani. Ila sindano haikupatikana.





Lakini ndege wengine walimwona Tai akipaa. Wakamwomba Kuku awaazime sindano ili nao wajishonee mabawa pia. Muda si mrefu ndege wakawa wamepaa na kuzagaa anga zima.



Ndege wa mwisho aliporudisha sindano aliyoazima, Kuku hakuwepo. Kwa hiyo watoto wake wakachukua sindano na wakaanza kuichezea. Walipochoka na mchezo wao, wakaiacha sindano kwenye mchanga.